

Statement of Support in Swahili

Tarehe: 10 Desemba 2025

Yah: BARUA YA NGUVU YA MAPENDEKEZO KWA
REV. DR. KRISTOPHER SCHONDELMAYER
UTEUZI WA CO-MODERATOR

Kwa heshima kubwa, imani kamili, na uthibitisho wa kiroho, naandika barua hii kumtoa mapendekezo ya juu kabisa Rev. Dr. Kristopher (Kris) Schondelmeyer kwa nafasi ya juu ya uongozi ndani ya Kanisa la Presbyterian (U.S.A.), pamoja na kumuunga mkono kikamilifu katika uteuzi wake kama mgombea wa nafasi ya Co-Moderator wa 227th General Assembly.

Ninamfahamu Rev. Schondelmeyer kwa miaka mingi katika nyanja za kitaaluma, huduma ya kanisa, na kwa uhusiano binafsi. Tulisoma pamoja katika Eden Theological Seminary, ambapo nilishuhudia kwa karibu kina cha maarifa yake ya kiteolojia, ubora wa kitaaluma, nidhamu, unyenyekevu, na kipawa kikubwa cha uongozi. Tangu wakati wa masomo, tayari alionesha wazi kuwa ni mtumishi wa Mungu mwenye uaminifu, maombi, ujasiri, na utambuzi wa hali ya juu wa kipastori.

Wakati wa huduma yake Toledo, Ohio, Mimi binafsi nilishuhudia maisha na huduma ya kanisa alilokuwa akihudumu. Kama Askofu Mstaafu mwenye uzoefu wa miaka mingi katika uongozi wa kiaskofu, utawala, na uendelezaji wa taasisi, nilimwangalia kwa karibu katika majukumu yake. Ninaweza kushuhudia bila mashaka uwezo wake katika:

- Huduma bora ya uchungaji wa watu wa Mungu
- Msingi imara wa Neno la Mungu na teolojia
- Uwezo thabiti wa uongozi wa kiutawala na kiutumishi
- Uwezo wa kuwaunganisha watu wa vizazi, tamaduni, na mitazamo mbalimbali
- Uaminifu mkubwa katika kweli, haki, uwajibikaji, upatanisho, na utakatifu

Rev. Schondelmeyer anadhihirisha kwa nadra mno mchanganyiko wa mamlaka ya kiroho yenye unyenyekevu, huruma yenye maamuzi thabiti, na maono yenye utekelezaji wa nidhamu. Haongozwi na tamaa ya binafsi, bali na shauku ya dhati ya kumtumikia Kristo na Kanisa Lake kwa uaminifu na ubora.

Kwa misingi ya ushuhuda wangu wa moja kwa moja wa huduma yake, malezi yetu ya pamoja ya kiteolojia, idhini zake za kikanisa, na uteuzi wake katika ngazi ya kitaifa ya kanisa, nampatia mapendekezo yangu ya juu kabisa, ya dhati, na yasiyokuwa na mashaka yoyote kwa Rev. Dr. Kristopher Schondelmeyer kwa nafasi yoyote ya uongozi ndani ya Kanisa la kimataifa.

Nina imani kamili kwamba popote Mungu atakapomweka, ataongoza kwa hekima, uaminifu, ujasiri, huruma, na mwelekeo sahihi wa kimkakati, kwa ajili ya kumleta Kristo heshima na kulijenga Kanisa Lake.

Bwana awaongoze katika mchakato wenu wa maamuzi kwa hekima na neema.

Askofu Isaiah Nathanieli Chambala
Askofu Mstaafu - Dayosisi ya Anglikana ya Kiteto, Tanzania
Mwanzilishi & Mshauri Mkuu - Bishop Chambala Foundation

Statement of Support in English

Date: 10 December 2025

RE: STRONG RECOMMENDATION FOR
REV. DR. KRISTOPHER SCHONDELMAYER
CO-MODERATOR CANDIDACY

It is with great honor, confidence, and spiritual conviction that I write this letter to strongly recommend Rev. Dr. Kristopher (Kris) Schondelmeyer for a position of significant leadership within the Presbyterian Church (U.S.A.), and to express my full support for his nomination as a candidate for Co-Moderator of the 227th General Assembly.

I have known Rev. Schondelmeyer for many years – academically, ministerially, and personally. We studied together at Eden Theological Seminary, where I witnessed firsthand the depth of his theological understanding, his academic excellence, discipline, humility, and remarkable leadership gifts. Even during his seminary years, it was already evident that he was a faithful servant of God—prayerful, courageous, and endowed with profound pastoral discernment.

During his ministry in Toledo, Ohio, I personally witnessed the life and ministry of the church where he served. As a Former Diocesan Bishop with extensive experience in episcopal leadership, governance, and institutional development, I carefully observed his:

- Outstanding pastoral and shepherding heart
- Strong biblical and theological foundation
- Proven administrative and strategic leadership capacity
- Ability to unite people across generations, cultures, and theological perspectives
- Deep commitment to truth, justice, accountability, reconciliation, and holiness

Rev. Schondelmeyer represents a rare balance of spiritual authority with humility, compassion with decisive leadership, and vision supported by disciplined execution. He is not motivated by personal ambition, but by a sincere desire to serve Christ and His Church with integrity and excellence.

Based on my direct personal experience with his ministry, our shared theological formation, his official ecclesiastical credentials, and his leadership at the national level of the church, I offer my highest, sincere, and unequivocal recommendation for Rev. Dr. Kristopher Schondelmeyer for any leadership position within the global church.

Wherever God places him, I am confident he will lead with wisdom, faithfulness, courage, compassion, and strategic clarity, for the glory of Christ and the strengthening of His Church.

May the Lord guide you in your decision-making process with wisdom and grace.

Bishop Isaiah Nathanieli Chambala
Former Bishop – Anglican Diocese of Kiteto, Tanzania
Founder & Senior Advisor – Bishop Chambala Foundation